

Msaada wa Kifedha kwa Bili za AHN

Allegheny Health Network (AHN) inaahidi kutoa huduma muhimu za kimatibabu kwa wagonjwa bila kujali kiasi wanachoweza kulipa. Ili kutimiza ahadi yetu, tunashirikiana na wagonjwa ili kuwasaidia kutimiza wajibu wao wa kifedha kwa huduma tunazotoa.

Nani anaweza kustahili kupata msaada wa kifedha kwa kulipiwa bili zake za AHN?

Allegheny Health Network inaweza kutoa msaada wa kifedha kwa bili za AHN kwa wagonjwa:

- Wasio na bima ya matibabu au wenye bima za afya zinazotoa huduma chache
- Wasiostahiki kupata Medicare au Medicaid
- Ambao ni raia wa Marekani au wakazi wa kudumu halali wa Marekani
- Wanaoishi katika eneo la msingi la huduma la AHN
- Ambao wanathibitisha uhitaji wao wa msaada wa kifedha kwa kutoa nyaraka zinazohitajika

Je, nitajuaje kama ninastahiki msaada wa kifedha?

Kila mgonjwa lazima aombe msaada wa kifedha kwa ajili ya kulipa bili za AHN. Ili kuomba:

- Pakua na uchapishe fomu ya maombi ya msaada wa kifedha ya Allegheny Health Network (fomu na maelekezo) kutoka kwenye tovuti ifuatayo, <https://www.ahn.org/financial-assistance-ahn-bills>.
- Jaza fomu na uiwasilishe pamoja na uthibitisho wa mapato unaohitajika.
- Ikiwa huwezi kupakua au kuchapisha fomu, unahitaji msaada wa kujaza ombi lako, au unahitaji msaada kuhusu mchakato wa kupata msaada wa kifedha kwa ajili ya hospitali zifuatazo: Allegheny General Hospital, Allegheny Valley Hospital, Canonsburg Hospital, Forbes Hospital, Grove City Medical Center, Jefferson Hospital, Saint Vincent Hospital, West Penn Hospital, Wexford Hospital, AHN Harmar Neighborhood Hospital, AHN McCandless Neighborhood Hospital, AHN Brentwood Neighborhood Hospital au AHN Hempfield Neighborhood Hospital. Tafadhali piga simu kwa Idara ya Ushauri wa Masuala ya Kifedha kupitia nambari 1-855-493-2500 au tembelea ofisi ya usajili wa wagonjwa katika hospitali ya AHN ambako ulipokea huduma.

- Tuma ombi kuomba kupata nakala ya bure ya Sera ya Msaada wa Kifedha na Fomu ya Maombi ya Allegheny Health Network kwa anwani iliyoorodheshwa hapa chini:

Idara ya Ushauri wa Masuala ya Kifedha

2 Allegheny Center, Suite 602

Pittsburgh, PA 15212

au tutumie barua pepe kwa FinancialAdvocates@AHN.org

AHN hukagua kila ombi la msaada wa kifedha bila kuchelewa. AHN itatuma barua kwa mgonjwa ikiwa maelezo zaidi yanahitajika.

Allegheny Health Network itamjulisha mgonjwa, au mdhamini wa mgonjwa, au mwakilishi wake kuhusu uamuzi huo, kwa maandishi.

Sera ya Msaada wa Kifedha ya Allegheny Health Network

Hospitali na madaktari wa Allegheny Health Network (AHN) wamejitolea kuboresha afya za wagonjwa wetu na jamii tunazozihudumia. Ni sera yetu kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wote bila ubaguzi, wakiwemo wale ambao wanaweza kuwa na ugumu wa kulipia huduma hizo kutokana na kipato chao kidogo. AHN huweka kikomo cha kiasi kinachotazwa kwa huduma za dharura au huduma nyingine za matibabu zilizo muhimu kimatibabu zinazotolewa kwa watu wanaostahili kupata msaada wa kifedha. Watu hawa hawapaswi kutozwa kiasi kinachozidi kile kinachotazwa kwa ujumla (AGB) kwa watu walio na bima ya afya. Ili kukidhi mahitaji ya jamii, AHN hutoa programu ya Msaada wa Kifedha.

Programu ya msaada wa kifedha ya AHN imefafanuliwa kwa kina katika Sera ya Msaada wa Kifedha na Ukusanyaji wa Madeni ya Allegheny Health Network, iliyoanza kutumika tarehe 1 Januari 2018. Sera hii inatumika kwa watoa huduma wa AHN na mashirika washirika yaliyo chini ya udhibiti wake, wakiwemo madaktari walioajiriwa. Huu hapa muhtasari wa sera hii, ambayo inafafanua:

- Ni nani anayestahili kupata msaada wa kifedha kutoka AHN, kwa kuzingatia miongozo ya viwango vya mapato?
- Ni huduma zipi za AHN zinazojumuishwa na zipi hazijumuishwi chini ya sera hii?
- Jinsi mgonjwa anavyoweza kuomba msaada wa kifedha kutoka AHN.

Nani anayestahili kupata msaada wa Kifedha?

Ni sera ya AHN kutoa msaada wa kifedha kwa wagonjwa ambao:

- Hawana bima ya matibabu au wana bima ndogo
- Wasiostahiki kupata Medicare au Medicaid
- Ambao ni raia wa Marekani au wakazi wa kudumu halali wa Marekani
- Wanaishi katika eneo kuu la huduma la AHN
- Ambao wanathibitisha uhitaji wao wa msaada wa kifedha kwa kutoa nyaraka zinazohitajika

Je, ni miongozo gani ya viwango vya mapato inayotumika kuamua kustahili kupata msaada wa kifedha?

Miongozo ya Serikali ya Viwango vya Umaskini ya mwaka 2026 kwa Majimbo 48 Yaliyoungana Kijiografia na Wilaya ya Columbia

Idadi ya Watu katika Nyumba	Kiwango cha Mapato	
	100%	200%
1	\$15,960.00	\$31,920.00
2	\$21,640.00	\$43,280.00
3	\$27,320.00	\$54,640.00
4	\$33,000.00	\$66,000.00
5	\$38,680.00	\$77,360.00
6	\$44,360.00	\$88,720.00
7	\$50,040.00	\$100,080.00
8	\$55,720.00	\$111,440.00

*Kulingana na mara mbili ya miongozo ya sasa ya umaskini. Kwa familia/nyumba yenye zaidi ya watu 8, ongeza \$5,680 kwa kila mtu wa ziada.

Ni huduma zipi zinazostahili kupata msaada wa kifedha?

Msaada wa kifedha unapatikana kwa wagonjwa wanaostahili kwa huduma zifuatazo:

- Huduma za matibabu ya dharura
- Huduma muhimu kiafya (si za hiari) kwa hali ya dharura ya kutishia maisha zinazotolewa nje ya Idara ya Dharura
- Huduma nyingine za matibabu zilizo muhimu kimatibabu, kulingana na tathmini ya kila kesi kivyake

Msaada wa kifedha kutoka AHN haupatikani kwa huduma kama vile:

- Huduma zinazochukuliwa kuwa “hazigharamiwi” na Medicare
- Huduma zinazochukuliwa kuwa si za lazima kimatibabu, ikiwemo lakini bila kuishia kwenye huduma zifuatazo:
 - Huduma za urembo
 - Huduma za hiari zinazohusiana na uzazi, kama vile urutubishaji wa yai nje ya mwili (IVF) au kufunga mirija ya mbegu za kiume na upasuaji wa kurejesha mirija hiyo katika hali yake ya awali
 - Upasuaji wa upandikizaji wa viungo vya mwili na huduma zinazohusiana
 - Upasuaji wa kupunguza uzito na huduma zinazohusiana
 - Huduma za tiba saidizi au tiba mbadala, kama vile tiba ya kuchoma sindano mwilini
 - Uchunguzi wa kawaida wa macho
 - Lenzi za macho zinazovalikiwa moja kwa moja kwenye jicho, vifaa vya kusaidia kusikia, na vipandikizi vya vifaa vya kielektroniki vinavyosaidia kusikia.
 - Kusisimua sehemu za ndani kabisa za ubongo kwa kutumia msukumo wa umeme
 - Uchujaji wa LDL kutoka kwenye damu
 - Huduma zinazogharimiwa na programu au ruzuku zisizo za AHN kama vile mpango wa Ryan White kwa ajili ya matunzo ya VVU/UKIMWI

Ninaombaje msaada wa kifedha kwa ajili ya bili za AHN?

Ili kuomba msaada wa kifedha kwa ajili ya bili za AHN, mgonjwa au mwakilishi wake lazima ajaze na kuwasilisha Fomu ya Maombi ya Msaada wa Kifedha ya Allegheny Health Network, pamoja na nyaraka zinazohitajika kuthibitisha mapato. Ombi na uthibitisho wa mapato lazima upokelewe na AHN ndani ya siku 240 tangu tarehe ambayo mgonjwa alipokea huduma za matibabu kutoka AHN.

Kwenye tovuti hii, <https://www.ahn.org/financial-assistance-ahn-bills>, sera ya msaada wa kifedha, muhtasari wa sera kwa lugha rahisi kueleweka, na fomu ya maombi zimetafsiriwa katika lugha zifuatazo:

- | | |
|------------------|----------------------|
| • Haitian Creole | • Kivietnamu |
| • Kinepali | • Kihispania |
| • Kirusi | • Kireno cha Brazili |
| • Kiukreni | • Kifaransa |
| • Mandarin | • Kiarabu |
| • Kiswahili | |

Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa za AHN

Ikiwa una maswali, unahitaji msaada wa kujaza fomu yako ya maombi, unahitaji nakala ya fomu iliyochapishwa kwenye karatasi, au ungependa kupata maelezo zaidi kuhusu bili yako ya Allegheny Health Network au programu yetu ya Msaada wa Kifedha, tafadhali tumia maelezo ya mawasiliano yaliyo hapa chini au nenda kwenye eneo la usajili wa wagonjwa hospitalini.

Kituo cha Huduma kwa Wateja: **1-833-684-0239**

Ushauri wa Masuala Kifedha: 1-855-493-2500 au tuma barua pepe kwa FinancialAdvocates@AHN.org

Allegheny General Hospital
320 East North Avenue
Pittsburgh, Pa 15212

West Penn Hospital
4800 Friendship Avenue
Pittsburgh, Pa 15224

Wexford Hospital
12351 Perry Hwy
Wexford, Pa 15090

Canonsburg Hospital
100 Medical Boulevard
Canonsburg, Pa 15317

Jefferson Hospital
565 Coal Valley Road
Jefferson Hills, Pa 15025

Allegheny Valley Hospital
1301 Carlisle Street
Natrona Heights, Pa 15065

Forbes Hospital
2570 Haymaker Road
Monroeville, Pa 15146

AHN Grove City
631 N. Broad Street Ext
Grove City, Pa 16127

Saint Vincent Hospital
232 West 25th Street
Erie, Pa 16544